NJIA YA MSALABA

Paraphrassed from MISALE YA WAUMINI

Br. Methodius Sakweli OSB
Njiro seminary 07655876446
22 February 2021



ndugusakwellus@gmail.com

(Mwendelezo kama juu)
2.Umekosa nini we YESU, Kushtakiwa bure kwa Pilato
Wenye kustahili hukumu, Si wewe, si wewe BWANA, ni sisi..

3. Ole Msalaba huo mzito, Apagazwa mwana mpenzi wa MUNGU.
Mwili waenea mateso, / Alipa, alipa madhambi yetu

4.Ona Muumba mbingu na nchi, Yupo chini mzigo wamwelemea,
Na mtu kiumbe chake kwa ukali, Ampiga, ampiga bila huruma.

5.Huko njiani we MARIA, Waonaje hali ya mwanao,
Ni damu tupu na vidonda, / Machozi, machozi yamfumba macho.

6.Kwa Simoni heri ya kweli, Mimi pia YESU nisaidie,
Kuchukua mzigo wa ukombozi, Kuteswa, kuteswa pamoja nawe
.
7.Uso wa YESU Malaika, Betlehemu walikuabudu,
Bahati yake Veronika, Kupangusa, kupangusa Mfalme wa Mbingu.

8.Wakimvuta huku na huku, Wauaji wanamchokesha bure,
Chini wanamtupa bado kwa nguvu, Aibu, aibu yao milele.

9.Wanawake wa Israeli, Msilie kwa sababu hiyo,
Muwalilie hao kwa dhambi, Upanga, upanga ni juu yao.

10.Mwokozi sasa ni ya tatu, Waanguka chini ya msalaba,
Katika dhambi za uregevu, Nijue, nijue kutubu hima.

11.Muje Malaika wa Mbingu, Funikeni mwiliwe kwa huruma,
Vidonda vyake na utupu, Askari, askari wamemvua.

12.Hapo MKRISTO ushike moyo, BWANA wako alazwa msalabani,
Mara miguu na mikono, Yafungwa, yafungwa kwa misumari

13.YESU mpenzi nakuabudu, Msalabani unapohangaika,
Nchi yatetemeka kwa hofu, Na jua, na jua linafifia.

14.Mama MARIA mtakatifu, Upokee maiti ya Mwanao,
Tumemwua kwa dhambi zetu, Twatubu kwake na kwako

15.Pamoja nawe kaburini, Zika dhambi na ubaya wa moyo,
YESU tuwe Wakristo kweli, Twakupa twakupa sasa mapendo

16.Katika roho yangu BWANA, Chora mateso niliyokutesa,
Nisiyasahau madeni, Na kazi, na kazi ya kuokoka.

ndugusakwellus@gmail.com